**THE UNIVERSITY OF DODOMA ACADEMIC STAFF ASSOCIATION (UDOMASA)**
IDS Building Office No. 206 & 207, P. O. Box 259, UDOM, Dodoma
Hotline +255743473121(Chairperson)/+255786145331(General Secretary)/+255621006921(Treasurer)
Email: udomasaudom@gmail.com

18 Julai, 2026

## TAARIFA YA NDANI KWA WANATAALUMA: KUHUSU KUSHIKILIWA KWA MWENZETU KITUO CHA POLISI

Ndugu Wanataaluma,

Siku ya tarehe 3/7/2026 mwanataaluma mwenzetu ndugu MELKISEDEKI KITUNZI KAIJAGE alipokea wito kupitia mkuu wake wa idara kuripoti kituo cha polisi UDOM. Baada ya kupokea wito huo, ndugu KAIJAGE aliutaarifu uongozi wa UDOMASA. Tarehe 8/7/2026 ndugu Kaijage aliripoti kituo cha polisi UDOM saa nne asubuhi akiambatana na Naibu Katibu Mkuu wa UDOMASA ambaye kitaaluma ni mwanasheria, na Ndg. Deusdedit Kivyiro ambaye ni mhadhiri msaidizi kutoka idara atokayo Ndg. Kaijage. Mkuu wa kituo alimjulisha kuwa wito huo ulitolewa na mkuu wa upelelezi mkoa (RCO). Maagizo hayo yalienda mbali zaidi ya wito na kwamba yalielekeza kuwa simu zake zichukuliwe na awekwe ndani na kwamba RCO atatuma polisi waje kumchukua.

Saa sita na dakika ishirini polisi waliotumwa na RCO walifika kituo cha polisi UDOM na kumchukua kumpeleka ofisi ya RCO na muda mchache baadae alipelekwa kituo kikuu cha polisi Dodoma. Mnamo saa kumi na nusu, ndugu Kaijage alichukuliwa na kupelekwa ofisi ya RCO kwa ajili ya kuchukuliwa maelezo ambapo maelezo yalichukuliwa mbele ya Naibu katibu mkuu wa UDOMASA na ndipo tulipobaini kwamba tuhuma anayotuhumiwa nayo ni kuhamasisha maandamano ya tarehe 7/7/2026 kwa njia ya mitandao ya kijamii. Baada ya kuchuliwa maelezo, tuliomba mtuhumiwa apewe dhamana maana kosa analotuhumiwa linadhaminika. Majibu ya ombi hilo yalitolewa na afande ASP Mwandika na alituambia kuwa anatambua kuwa kosa linadhaminika lakini kuna maagizo kutoka juu kuwa arudishwe mahabusu. Hivyo Ndg. Kaijage alirudishwa mahabusu katika kituo kikuu cha polisi Dodoma.

Siku ya tarehe 9/7/2026 Ndg. Kaijage alihamishwa kutoka mahabusu ya kituo kikuu cha polisi Dodoma na kupelekwa kituo kidogo cha polisi Chang'ombe. Kwa siku zote hizi uongozi wa UDOMASA uliendelea kufuatilia kwa ukaribu kadhia hii na kushirikiana na ndugu wa Ndg. Kaijage. Uongozi, kupitia mwanasheria na Naibu katibu mkuu uliendelea kusukuma ombi la kupatiwa dhamana.

Siku ya tarehe 10/7/2026, baada ya kujiridhisha kuwa ombi la dhamana limekwama, uongozi wa juu wa UDOMASA uliamua kutumia njia ya mahakama ili kuwezesha mwezetu kupata dhamana. Siku ya tarehe 12/7/2026 tulifungua kesi mahakama kuu kanda ya Dodoma ambapo jana tarehe 17/7/2026 kesi ilisikilizwa kwa mara ya kwanza. Baada ya kusikilizwa mara mbili saa tatu asubuhi na saa nane na nusu mchana, kesi iliahirishwa na itasikilizwa tena siku ya jumanne tarehe 21/7/2026 saa tatu asubuhi, mahakama kuu Dodoma.

UNIVERSITY OF DODOMA ACADEMIC STAFF ASSOCIATION
P. O. BOX 259
DODOMA-TANZANIA
UDOMASA

CamScanner

THE UNIVERSITY OF DODOMA ACADEMIC STAFF
ASSOCIATION (UDOMASA)
IDS Building Office No. 206 & 207, P. O. Box 259, UDOM, Dodoma
Hotline +255743473121(Chairperson)/+255786145331(General Secretary)/+255621006921(Treasurer)
Email: udomasaudom@gmail.com

UDOMASA inatambua na kusimamia haki za wafanyakazi, na tunapinga na kulaani vikali ukiukwaji wowote wa taratibu za kisheria unaomnyima mfanyakazi uhuru wake. Chini ya sheria za nchi yetu, mtuhumiwa anapaswa kufikishwa mahakamani ndani ya saa 24. Jumuiya yetu inafuatilia kwa karibu sana suala hili. Haki za mfanyakazi ni haki za msingi za kibinadamu na hatutafumbia macho ucheleweshaji wowote usio na tija.

Tunawasihi wanataaluma wote kuwa watulivu wakati taratibu za kisheria zikiendelea kuchukua mkondo wake kupitia mahakama na vyombo vya dola.

Tutawajulisha maendeleo yoyote yatakayojitokeza, ikiwa ni pamoja na hatua ya dhamana au kufikishwa mahakamani kwa mwenzetu.

***Mshikamano Daima***

UNIVERSITY OF DODOMA ACADEMIC STAFF ASSOCIATION
P. O. BOX 259
DODOMA-TANZANIA
UDOMASA

Isaac Mahenge,
Katibu mkuu UDOMASA.

CamScanner